

# Kibandiko cha shukrani

Maandiko yanatufundisha kuwa na shukrani (ona Zaburi 100:4). Unaweza ukawa na burudani na ukawa mwenye shukrani unapocheza mchezo huu!



1. Tafuta sehemu ya wazi ambako unaweza kukimbia. Chagua sehemu moja iwe "Eneo la Shukrani."
2. Kila mtu anaweza kumgusa mwengine! Unapokuwa umeguswa, weka mkono kwenye eneo uliloguswa. Unaweza bado ukawagusa watu kwa mkono wako mwengine
3. Unapoguswa mara ya pili, weka mkono wako huo mwengine kwenye sehemu ya pili uliyoguswa.
4. Unapokuwa umeguswa mara ya tatu nenda Eneo la Shukrani na sema vitu vitatu ambavyo unashukrani kwavyo. Utakapokuwa umekwishavitaja vitu vitatu, unaweza kujunga na mchezo tena.

Unafikiri twiga huyu  
anasema nini?  
Andika na utuelezee!  
Geuza kwenye jalada  
la nyuma ili kuona  
jinsi ya kufanya.

